**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

**HOTUBA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA WANAWAKE HABARI NA UTALII YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA BAJETI YA WIZARA YA VIJANA UTAMADUNI SANAA NA MICHEZO - 2020/2021**

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

**Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote naomba kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia afya na uwezo kwa siku ya leo kuweza kuendelea kutekeleza majukumu yetu ya kuwatumikia wananchi na nchi yetu kwa ujumla. Napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii, ili niweze kutoa maoni ya Kamati yangu katika Baraza lako hili tukufu kuhusiana na Makadirio ya bajeti ya Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Napenda kwa aina ya pekee kutoa shukurani zetu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri , Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa wizara hii kutokana na mashirikiano makubwa waliyoyaonesha wakati wote wa kazi za Kamati.
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Vile vile, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kwa mashirikiano ya pamoja waliyoyaonesha ndani ya Kamati yetu pamoja na jitihada yao ya kufanya kazi kwa bidii bila ya kuchoka.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba sasa niwatambue Wajumbe wa Kamati hii ambao kwa mashirikiano makubwa wameiwezesha Kamati yetu kufanya kazi yake vizuri na kwa ufanisi mkubwa. Wajumbe wenyewe ni kama wafuatao:-

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mussa Foum Mussa | M/Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Makame Said Juma | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Omar Seif Abeid | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Mjumbe |
| *7.* | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| *8.* | Ndg. Himid Haji Choko | Katibu |
| *9.* | Ndg. Mussa Issa Mussa | Katibu |
| *10.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Msaidizi |
| *11.* | Ndg. Azmina Hamad Khamis | Msaidizi |

## MAKUSANYO YA WIZARA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu inaendelea kuipongeza Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kuvuka lengo la makusanyo ya Mirabaha ya wasanii na wabunifu na kufikia asilimia **119%.** Hili ni jambo jema, na tunawaomba watendaji wazidi kulisimamia hili, ili makusanyo zaidi yaweze kupatikana. Hata hivyo, Kamati inaiomba wizara kuongeza bidii zaidi ya makusanyo yanayoingia Mfuko Mkuu wa Hazina kwani asilimia **48%** iliyofikiwa bado ni ndogo.

**Mheshimiwa Spika**, tukisoma Kiambatanisho Namba **1B** kinachohusu Mapato ya Wizara katika Kitabu cha Mheshimiwa Waziri Ukurasa wa 62 tunashuhudia mtiririko halisi wa mapato hayo. **Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitumia muda Mrefu kujadili hali hii na wizara imejitetea kwamba, kuanguka kwa mapato haya kunatokana na kufungwa kwa kumbi nyingi za burudani hasa katika hoteli za kitalii kwa baadhi ya Mikoa. Hivyo, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii inazishauri Mamlaka zote zinazohusika na kadhya hii kukaa pamoja na kutafuta njia muwafaka ya kuhakikisha serikali inaingiza mapato kupitia Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu kwa kuwepo soko la kazi za sanaa na huku tukiwa na tahadhari

kubwa ya Uhifadhi wa Utamaduni kulingana na silka na desturi za Mzanzibari.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara pia ilijitetea kwamba, kuanguka kwa makusanyo kupitia Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA)
kunatokana na kushuka kwa ari na utamaduni wa kusoma majarida na machapisho ya Baraza hilo. Tunawaomba sana BAKIZA kutilia maanani Msemo wa wahenga kwamba "***Hadaa yaghilibu shujaa*** " unaomanisha kuwa, Mbinu hupelekea ufanisi mkubwa wa mambo, hivyo Kamati yetu tunaihimiza wizara kuongeza juhudi ya kukikuza Kiswahili na kukifanya kuwa bidhaa pamoja na kubuni njia nyengine za mapato kama vile huduma za tafsiri na ukalimani.

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA VIJANA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu kwa mara nyengine tena na kwa dhati kabisa inaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa juhudi kubwa anazozichukuwa pamoja na kuumwa na kukereketwa sana na Maendeleo ya Vijana hapa nchini. Tunaendelea kuthamini sana juhudi hizo na tunaendelea kuwasisitiza wale wote waliopewa dhamana ya kusimamia masuala ya vijana tuunge mkono juhudi za

Mheshimiwa Rais, ili malengo yaliyokusudiwa katika kuwaendeleza vijana wetu yaweze kufikiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu imeridhika na fedha zilizotengwa kwa ajili ya Kutekeleza Programu ya Maendeleo ya VIjana hapo mwakani, lengo likiwa ni kuwajengea uwezo vijana wetu ili wajiongezee ajira na kukuza vipato vyao.

**Mheshimiwa Spika,** Kuhusiana na Mradi wa Kilimo cha Pilipili, Kamati yangu kwa furaha kubwa inaishukuru sana Serikali yetu sikivu, ambapo baada ya ushauri wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake Habari na Utalii pamoja na Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, hatimae Serikali iliunda Kamati ya Kitaalamu ya kuchunguza Kadh-ya nzima ya Mradi wa Vijana wa Kilimo cha Pilipili na tayari ripoti hiyo imewasilishwa Serikalini kama ilivyoripotiwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri hivi punde.

**Mheshimiwa Spika**, kwa umuhimu wa Mradi huu na kadhya yenyewe, naomba niyakariri tena yatokanayo na Ripoti hiyo kama ifuatavyo; "Pamoja na mambo mengine Serikali imetoa maagizo yafuatayo:-

i. Mradi wa pilipili usimamiwe na Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi pamoja na Shirika la ZSTC kwa ajili ya kupata ushauri wa kitaalamu wa kilimo na masoko;
ii. Kuangalia upya makubaliano yaliokuwepo ya mkataba kati ya ZSTC, "Kampuni ya Vegrab Organic Farming Limited" na vijana; na
iii. Kuhakikisha pilipili zinalimwa kwenye maeneo ambayo yamethibitishwa kitaalamu na taasisi zetu za kilimo Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii inakubaliana kabisa na maagizo hayo ya serikali pamoja na kuunga mkono yale yote yaliyopendekezwa na Kamati ya kitaalamu iliyochunguza mradi huo.

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu inaunga mkono Shabaha Kuu iliyokusudiwa katika Programu hii ambayo ni kuwa na utamaduni na sanaa inayowaendeleza wasanii, ili kuweza kujiinua kiuchumi na kupunguza umasikini pamoja na kuifanya michezo kuwa sehemu ya ajira na kujenga afya za wananchi wetu. Tunawaomba waheshimiwa wajumbe kukubaliana na maombi ya wizara ya kuwaidhinishia fedha zote walizomba kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii.

## UIMARISHAJI WA MIUNDOMBINU YA MICHEZO

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo kupitia bajeti ya Mwaka ujao, pamoja na mambo mengine ya kuimarisha michezo pia imeahidi kuendelea kuviimarisha viwanja vya Amani, Gombani, Mao Zedong na viwanja vya Wilaya. Tunaunga mkono azma hii, lakini tunahimiza mkazo zaidi ukawekwa katika kukihami kiwanja cha Gombani kwani hivi sasa hali yake sio nzuri kulingana na hadhi na matumizi ya kiwanja chenyewe.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu katika ziara zake za mwisho Kisiwani Pemba ilishuhudia sehemu nyingi za uwanja huo ambazo zinahitaji masawazisho ikiwemo mfumo wa taa za kwenye minara, miundombinu ya vyoo na maji pamoja na majukwaa.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa, Kamati yangu inakupongeza kwa dhati wewe Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mhe. Zubeir Ali Maulid, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Baraza , Waheshimiwa Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu na bila ya kumsahau Katibu wa Baraza la Wawakilishi Ndg. Raya Issa Msellem na sekreratiati yake yote kwa kuiwezesha vyema Kamati yetu kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo sasa nachukuwa fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii na niwaombe waheshimiwa wajumbe wote kuijadili kwa kina na hatimae kuipitisha Bajeti hii, ili kumuwezesha Mheshimiwa Waziri kutekeleza mipango na shabaha zake kama alivyojipangia.

**Mheshimiwa Spika**, naomba Kuwasilisha.

Ahsante.

**..........................**
**(Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis)**
**Mwenyekiti**
**Kamati ya Maendeleo ya Wanawake Habari na Utalii,**
**Baraza la Wawakilishi.**
**Zanzibar.**